Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

**Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)**

**ISSN: 2663-9289**

**Volume: 02 Issue: 01 | Aug-2020|**
**Received: 05.08.2020; Accepted 09.08.2020; published on 31.08.2020 at www.editoncpublishing.org**
**Poyi, J.C., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal***

# Usawiri wa Ukombozi katika Diwani ya Euphrase Kezilahabi *ya Kichomi*: Mtazamo wa Kidhanaishi

**Chibayi Jason Poyi[1]; Dkt. Sheila Pamela Wandera-Simwa[2]**
**[1,2]Idara ya Lugha, Fasihi na Isimu, Chuo Kikuu cha Laikipia, Kenya**
**Main Author Email: jasonchibayi@gmail.com**

## IKISIRI

Makala hii inakusudia kuonyesha namna ukombozi ulivyosawiriwa kama sehemu ya falsafa ya Euphrase Kezilahabi katika diwani yake ya *Kichomi.* Euphrase Kezilahabi ni mwandishi nguli wa mashairi aliyeasi magwanda ya umapokeo. Mojawapo wa sifa bainishi ya falsafa ya Kezilahabi ni ukombozi, ambayo huifanya kuwa falsafa ya uhuru yenye tafsiri nyingi ambazo ndizo msingi wa makala hii. Tahakiki nyingi kuhusu diwani hii imeshughulikia falsafa ya maisha ya Kezilahabi pasipo kuangazia usawiri wa ukombozi kama sifa bainishi ya mhimili wa uhuru. Makala hii itafafanua usawiri wa ukombozi huu kwa kutumia nadharia ya Udhanaishi iliyoasisiwa na Jean Paul Satre (1970). Sampuli ya makala hii iliteuliwa kimaksudi. Data ya kimsingi itakusanywa kwa njia ya kusoma mashairi katika diwani teule na makala mengine yanayohusiana nayo. Makala hii itachukua muundo wa kimaelezo na data itakayokusanywa itafafanuliwa kwa njia ya maelezo kwa kuegemeza kwenye mhimili wa uhuru wa nadharia ya Udhanaishi. Uchanganuzi wa data wa makala hii utaongozwa na mbinu ya uhakiki matini. Kwa kuwa diwani za mashairi ya Kezilahabi zimekuwa taaluma ya mijadala mipana, makala hii itakuwa mchango mkubwa kwa mijadala hiyo. Itawasaidia wanataaluma ya ushairi kuelewa namna Kezilahabi anavyousawiri ukombozi wa binadamu kwenye mashairi ya diwani ya *Kichomi*.

**Maneno muhimu:** Uhuru, Ukombozi, Falsafa, Maisha, Udhanaishi

-----------------------------------------------------------------***-----------------------------------------------------------------

**How to cite this article in APA (6th Edition)**

Poyi, C. J. & Wandera-Simwa,S. (2020). Usawiri wa ukombozi katika diwani ya Euphrase Kezilahabi *ya kichomi*: mtazamo wa kidhanaishi. *Editon Cons. J. Kiswahili,* 2(1), 110-109.

-----------------------------------------------------------------***-----------------------------------------------------------------



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | Aug-2020|
Received: 05.08.2020; Accepted 09.08.2020; published on 31.08.2020 at www.editoncpublishing.org
Poyi, J.C., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

## Utangulizi

Ushairi wa Kezilahabi umeonyesha namna anavyoyaelewa maisha ya wanajamii pamoja na mazingira yao. Uelewa huu unamfanya Kezilahabi kubainisha falsafa yake ya maisha pamoja na msimamo wake kuhusu maisha hayo ya jamii. Miongoni mwa mambo anayoyashughulikia katika ushairi wake ni maana ya maisha. Msimamo wake Kezilahabi kuhusu maisha umeathiriwa kwa kiasi kikubwa na falsafa ya udhanaishi. Nadharia ya Udhanaishi ambayo imehusishwa katika uhakiki huu hujishughulisha zaidi na dhana ya maisha yenye swali la kimsingi; Maisha ni nini? Swali ambalo binadamu huwa mbioni kulijibu ili ajikomboe. Kezilahabi ametathmini kwa uketo na uluwa nafasi ya binadamu ulimwenguni na juhudi zake za kujikomboa kutoka kwa silisili za maisha yanayomtesa. Hata hivyo, falsafa ya maisha anayoisawiri Kezilahabi katika mashairi yake, inaonyesha kwamba juhudi za binadamu za kujikomboa hazimfikishi popote kutokana na ukweli kwamba uhuru wanaousaka ni nadra kuupata. Maisha anayoyasawiri Kezilahabi yanatamausha kwa sababu hayatoi mwanga kuhusu uwezekano wa hali ya binadamu kubadilika na kuwa nzuri zaidi. Wa aidha, ukombozi wa Kezilahabi ni wa kibinafsi unaomtafakarisha binadamu katika upweke wake. Diwani ya Kezilahabi ya *Kichomi* ina mashairi yanayomsawiri binadamu akiwa yupo katika juhudi za kusaka maana ya kuishi kwake. Ni dhahiri kwamba maisha ni fumbo ambalo linamtesa binadamu. Fumbo hili limemfanya binadamu kuwa mfungwa wa maisha. Hivyo makala hii ni mchango kwa taaluma ya mijadala ya kiusomi kuhusu ushairi wa Kezilahabi.

### Mapitio ya Maandishi

Ijapokuwa mashairi ya Kezilahabi yametafitiwa sana, ni dhahiri kuwa ukombozi kama sifa bainishi ya falsafa ya Kezilahabi haujaangaziwa kwa kina. Tafiti za awali zilijikita katika matumizi ya lugha, mifumo ya siasa, uchumi, utawala na dhana ya maisha kwa jumla. Omary (2011) katika mahojiano yake na Senkoro (2010) anasema kwamba wakati ushairi wa wahafidhina ulikuwa unatilia mkazo ushairi wenye kuadili na kuabudu kama masuala kuu, Kezilahabi alikuwa akiandika kuikosoa mifumo ya siasa, utawala na uchumi iliyokuwa imezorota kama njia ya kuonyesha kutoridhishwa kwake na viongozi wa umma. Senkoro anasema kuwa Kezilahabi pia aliyaangazia maisha ambayo wananchi walikuwa wameanza kuyaona kama hayana maana tena. Japo Senkoro (2010) hakuyahimimihili mawazo haya kwenye nadharia ya uhakiki, makala hii imenufaika kwayo kwa sababu yameibua dhana ya maisha kutoridhisha inayomsukuma binadamu kujikomboa. Hili lilimshughulisha Kezilahabi kwenye kazi zake, diwani ya *Kichomi* ikiwemo.

Karama na Mwamzandi (2019) katika makala yao ya "ushairi wa Kezilahabi ni ushairi wa Nabhany: Ushahidi kutoka uchanganuzi wa umbo la shairi la wanajadi," wanakariri hoja kwamba ushairi wa Wanamapinduzi ni ushairi wa Wanajadi. Wanaainisha mashairi ya Kiswahili kwa vigezo vilivyotolewa na Mwanajadi Nabhany, na kubainisha kwamba umbo la shairi linatokana na mpangilio maalumu wa sauti. Kwa kuchanganua umbo la shairi moja la Kezilahabi kupitia kigezo cha bahari ya utumbuizo, ambayo Nabhany ameiorodhesha kuwa bahari mojawapo ya mashairi ya kijadi ya Kiswahili, Karama na Mwamzandi (2019) wanadai kwamba, ushairi wa Kezilahabi una sifa zote, ama karibu zote, za bahari hiyo na hivyo kuhitimisha kuwa ushairi wa Kezilahabi ni ushairi wa Wanajadi. Ujadi huu unatokana na sifa za dhima, matumizi ya lugha na wahusika katika mashairi haya. Utafiti huu unatofautiana na wa sasa kwa sababu ulilenga kuonyesha ushairi wa Kezilahabi kama ushairi wa jadi wa Nabhany.

Mulokozi (1992) anamsawiri Kezilahabi kama mkosoaji wa jamii anayedadisi kila kitu kuanzia kwa mifumo jadi ya



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | Aug-2020|
Received: 05.08.2020; Accepted 09.08.2020; published on 31.08.2020 at www.editoncpublishing.org
Poyi, J.C., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

jamii na Ujamaa, dini, mfumo wa elimu ya kimagharibi na falsafa za kisiasa na suala la maisha. Anamwona Kezilahabi kama msanii mwenye fikira komavu anayeangazia masuala yaliyozoeleka katika jamii kwenye kazi zake kwa mtazamo binafsi wa kidhanaishi, na kufanikiwa kuweka wazi wasiwasi na mtanziko wa masuala yanayowakumba wanadamu katika jamii. Utafiti huu wa Mulokozi (1992) umenufaisha makala hii kwa kuwa umeibua dhana ya falsafa ya maisha ya Kezilahabi anayoiangazia kwa mtazamo wa kidhanaishi ambayo ndiyo msingi wa utafiti huu.

Ushairi wa Kezilahabi una matumizi ya lugha rahisi ya mazungumzo, lakini iliyosheheni tamathali hasa, ishara, sitiari, taswira na udokezi (Mulokozi 2008, 2017). Ndani ya lugha hii, Mulokozi anasema kwamba, Kezilahabi amefumbata falsafa nzito ya maisha. Mulokozi (2008) anasema kwamba, mojawapo wa sifa za kifani ambayo wasomaji wa Kezilahabi huihusisha na uandishi wake ni ile ya ucheshi. Anadai kwamba mwandishi humchochea msomaji wake acheke na kujicheka, na baadaye akereke kwa kuutambua ulimwengu wake. Anasisitiza kwamba ucheshi huo ni nyenzo muhimu na kubwa ya tashtiti inayotokeza katika sanaa ya mwandishi huyu. Kadhalika, anasema kwamba ucheshi huu pia ni nyenzo kuu ya kufikia ule upeo wa furaha ambao unatokana na burudani ya kisanaa. Anasema kwamba Kezilahabi anatumia lugha ya aina hii kwa sababu ndiyo moyo wa ushairi wa jadi wa kiafrika. Kwa mujibu wa Mulokozi (2017), Kezilahabi anatumia taswira za vijijini, majini (mamba, mashua), mimea na mbegu, visasili na visakale, ngoma na duara kuumba maudhui yake. Japo Mulokozi alidhamiria kuangazia matumizi ya lugha katika ushairi wa Kezilahabi, anagusia falsafa yake ya maisha anayoifumbata katika lugha hiyo na kuzua ilhamu zaidi ya makala hii.

Akihakiki taswira ya maji katika ushairi wa Kezilahabi, Ranne (2006) anadai kwamba, taswira ya maji anayoibua Kezilahabi inaashiria maisha, mahangaiko na migongano mitupu ya maisha ya binadamu. Ranne anafasiri taswira za kukauka na kuwa yabisi kama zinaoonyesha kifo. Aidha, taswira ya matone ya maji inaonyesha miaka ya kuishi. Ranne anabainisha kwamba, kadri mzungumzaji katika shairi anavyozidi kukua ndivyo maji yanavyozidi kusonga. Anadai kuwa taswira ya kidimbwi cha maji inaonyesha wasiwasi na hatari ya maisha ya mwanadamu. Ijapokuwa Ranne alihakiki taswira ya maji, utafiti wake unaibua falsafa ya maisha inayomshughulisha Kezilahabi katika diwani ya *Kichomi*.

Kezilahabi amechota maudhui yake kutoka kwenye jamii, mifumo ya siasa na matatizo ya kisaikolojia. Masuala haya ndiyo yamekuwa nguzo inayohimili fasihi ya Kiafrika ya enzi hizi. Hata hivyo, mtunzi huyu ni msanii wa pekee kwa namna yake ya kutumia jazanda. Watafiti wengi wametaja umuhimu wa ishara na picha katika tungo za Kezilahabi. Acquaviva (2004:69) anaeleza kuwa ni taswira, sitiari na mafumbo ndiyo yanayofanya mashairi ya Kezilahabi kuwa tofauti. Mlacha (1987) anaona ishara na picha kuwa muhimu katika kazi zake Kezilahabi kwa kuwa zinasawiri mtindo unaoendeleza muundo wa riwaya zake. Ijapokuwa maoni ya watafiti hawa yanashughulikia matumizi ya lugha katika kazi za Kezilahabi, utafiti wao unadhihirisha nafasi ya lugha katika falsafa ya maisha ya Kezilahabi.

Kwa mujibu wa Senkoro (2006), mashairi ya Euphrase Kezilahabi yana matumizi mengi ya maumbo ya fasihi simulizi, suala ambalo linayafanya mashairi kwenye diwani zake kuwa na maumbo ya Kiafrika zaidi kuliko yale ya Kimagharibi kama ilivyo katika baadhi ya kazi za fasihi. Senkoro anadahili kwamba, Kezilahabi ameandika ushairi pia kwa kutumia mbinu za kimasimulizi kama vile ucheshi, matumizi ya picha, ishara, taswira, taharuki na uradidi. Kwa kufanya hivi, Senkoro amedokeza vigezo vya lugha ambavyo ni dhahiri katika falsafa ya Kezilahabi. Senkoro



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | Aug-2020|
Received: 05.08.2020; Accepted 09.08.2020; published on 31.08.2020 at www.editoncpublishing.org
Poyi, J.C., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.,* Double –Blind Peer Reviewed Journal

(2006) alilenga kuainisha vigezo vya lugha vinavyoifumbata falsafa ya maisha ya Kezilahabi, makala hii imehakiki ukombozi kama sifa na sehemu ya falsafa hiyo kwenye mashairi ya diwani ya Kichomi.

Katika makala yake, "Kuwako na Wakati: Mipaka ya Matumizi ya Lugha Katika Mashairi ya Kezilahabi," Gaudioso (2014) alieleza nafasi ya matumizi ya lugha kwenye diwani za Kezilahabi. Kwenye utangulizi wa utafiti huu, Gaudioso (2014) anasawiri jinsi Tanzania ilivyokuwa na changamoto mbalimbali za lugha ya fasihi na ambayo Kezilahabi anaitatua kwenye fasihi yenyewe, kifalsafa na kishairi, na kuanzisha kurasa mpya kwa fasihi ulimwenguni. Gaudioso anafafanua falsafa ya Kezilahabi kilinganishi na kiutafsiri, ili kuonyesha namna vipengele vya sitiari na mafumbo vya Kezilahabi vinavyoingiliana na vile vya Heidegger na Nietzsche. Ijapokuwa makala ya Gaudioso (2014) yaliangazia falsafa ya Kezilahabi kilinganishi na kiutafsiri, yanadokeza utafiti zaidi kuhusu ukombozi wa binadamu katika mawanda yote ya maisha.

Omary (2011) anahakiki siasa katika diwani ya *Karibu Ndani* na *Dhifa* na kusema kwamba usawiri wa dhamira za kisiasa katika diwani hizi umejengwa katika vipengele vya fani. Anachunguza vipengele vya usimulizi, ucheshi, taswira na ishara, mwingiliano tanzu, wahusika, tanakali sauti na dhana ya ukimya na kisha kuonyesha namna vinavyosaidia kuibusha dhamira za siasa katika diwani teule. Kulingana na Omary (2011), ni sharti mhakiki aunde muunganno wa vipengele hivi vya fani na kuona namna vinavyokamilishana katika kujenga dhamira na maudhui ili kupata maana ya shairi. Ingawa utafiti wake unashughulikia siasa katika diwani teule, Omary (2011) ametuelewesha badhi ya vipengele vya lugha anavyovitumia Kezilahabi katika ujenzi wa maudhui kwenye mashairi yake, falsafa ya maisha ikiwemo.

Hassan (2013) anayalinganisha kifani mashairi ya Euphrase Kezilahabi na Haji Gora Haji. Katika utafiti wake anabainisha kuwa waandishi hawa wana mitindo ya kipekee katika uandishi na utunzi wa mashairi yao, mitindo ambayo huwapa upekee katika kuwasilisha ujumbe wao. Baadhi ya vipengele vya fani alivyohakiki ni mbinu za lugha kama vile ishara, taswira, ucheshi miongoni mwa mbinu nyingine. Katika utafiti wake, Hassan anabainisha kuwa wasanii hawa wawili walitumia sana ucheshi, ishara, taswira na lugha ya mkato katika kuwasilisha ujumbe wao. Utafiti huo wa Hassan (2013) pia ulidokeza maudhui yaliyojitokeza katika mashairi hayo na kubainisha kuwa dhamira zilizojitokeza katika mashairi hayo zinasawiri hali halisi ya maisha ya jamii waliyoiandikia. Ijapokuwa utafiti wa Hassan ni wa kulinganisha fani na maudhui, umeibua usawiri wa maisha yenye kutamausha ambayo ni sehemu ya falsafa ya Kezilahabi kwenye diwani ya Kichomi inayohakikiwa.

Akihakiki uhamishaji na kuandika upya uhuru katika mashairi ya Kezilahabi, Gaudioso (2015) anachunguza namna athari za wanafalsafa wa Kijerumani Martin Heidegger na Friederich Nietzsche zinavyojitokeza katika mashairi ya Kezilahabi. Gaudioso (2015) anabainisha kwamba wanafalsafa hawa walimwathiri Kezilahabi sio tu katika maudhui na mtindo wa kuandika, bali pia katika fikira za ukombozi na uhuru wa mwafrika. Kwenye makala hii, Gaudioso (2015) anahakiki mashairi ya Kezilahabi kwa kuzingatia kigezo cha uhuru wa falsafa ya Nietzsche ili kuonyesha uhusiano na mlingano wacho na wa dhana fulani za falsafa ya Kezilahabi. Gaudioso alijikita katika matumizi ya ishara na istiari katika makala yake ambayo yanazionyesha kama kigezo muhimu cha falsafa ya Kezilahabi na ile ya Nietzsche katika kuwasilisha ujumbe. Anadai kwamba Kezilahabi anatumia sana istiari na ishara kwa sababu inafanya watu kuuona na kuhisi ushairi wake. Ijapokuwa haya yalikuwa makala linganishi ya falsafa ya Nietzsche katika mashairi ya Kezilahabi,



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | Aug-2020|
Received: 05.08.2020; Accepted 09.08.2020; published on 31.08.2020 at www.editoncpublishing.org
Poyi, J.C., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, Double –Blind Peer Reviewed Journal

yanaibua dhana ya ukombozi na uhuru inayochochea kufunua ukombozi huu kama sehemu ya falsafa ya maisha ya Kezilahabi.

Mapitio haya ya kazi tangulizi, yameonyesha kuwa hakuna utafiti wa moja kwa moja uliochunguza ukombozi kama sifa bainishi ya falsafa ya maisha katika diwani ya *Kichomi* ya Euphrase Kezilahabi. Mapitio hayo yameonyesha kuwa upo mwanya wa kiusomi unaopwaya katika nyanja hiyo na kuibua haja ya kufanywa kwa utafiti huu ili kuziba mwanya huo, na hivyo kuiendeleza fasihi ya Kiswahili kwa ujumla; na hasa katika ushairi andishi.

**Msingi wa nadharia**

Nadharia ambayo imehimili makala hii ni ile ya Udhanaishi. Nadharia hii ni muhimu katika kuchunguza maisha ya binadamu na namna anavyowajibikia hali yake duniani. Udhanaishi ni falsafa ya maisha ambayo hutoa taratibu za kuelezea hali na maisha ya mwanadamu, mahali pake na jukumu lake katika dunia pamoja na mahusiano, au ukosefu wa mahusiano hayo na Mungu. (Sartre, 1970; Wamitila, 2002; 2003; TUKI, 2006; Njogu na Chimerah, 1999; Njogu na Wafula 2007: Reynolds, 2006). Wadhanaishi humtazama binadamu kama kiumbe pweke na aliyejitenga katika ulimwengu usio na maana na wenye ukatili. Wanashikilia kwamba binadamu anawajibikia matendo yake na kwamba yuko huru kuchagua hatima ya maisha yake. Mwasisi mkuu wa nadharia hii ni Jean`Paul Sartre (1970). Sartre alitoa mwelekeo kuhusu maisha ya binadamu kupitia kwa falsafa yake ya Udhanaishi iliyodhamiria kujibu swali la, "Ni nini maana ya kuishi?" alilodai ndilo la msingi.

Cooper (2004) na Wamitila (2002) wanaainisha mihimili ya nadharia hii kuwa ni pamoja na mtu duniani, uhuru wa mtu, vizingiti au matatizo halisi yanayomsibu mtu binafsi katika hali ya kukwepa imani ya kijonzi juu ya maana ya maisha, suala la kuwepo au kutokuwepo kwa Mungu na tanzia inayokurubiana na maisha ya binadamu. Wanaonyesha kuwa jitihada za binadamu za kujitafutia ukweli wa maisha kila mara hutiwa kikomo na mauti. Ni muhimu kutaja kwamba makala hii imehusisha nguzo ya uhuru katika kuchanganua data yake ya kimsingi. Mhimili huu husawiri ukombozi anaotafuta binadamu kuwa wenye mipaka. Kwenye falsafa yake ya maisha, Kezilahabi anamsawiri binadamu akiwa kwenye mandhari ya kutisha akisaka uhuru wake. Nafasi ya mandhari haya ya binadamu inasisitizwa na Mbatiah (1997) anapodai kwamba wasanii hutumia mandhari katika fasihi ya kidhanaishi kubainisha msimamo wao kwamba ulimwengu ni wa kinasibu, duni na wa kukatisha tamaa, na kwamba mandhari yanazua hisia za uchovu, huzuni na kukatisha tamaa. Hivyo basi, mhimili huu umetumika kuonyesha namna harakati za ukombozi wa binadamu zinavyochosha, kuhuzunisha na kukatisha tamaa, sifa ambazo zinatambulisha falsafa ya maisha ya Kezilahabi.

**Usawiri wa ukombozi katika diwani ya *Kichomi***

**Ukombozi ni mateso**

Kezilahabi sawa na wadhanaishi wengine, hutilia mkazo mateso yanayomkumba binadamu katika harakati za kujikomboa. Mashairi yake ya diwani ya *Kichomi yanaangazia* masuala dhanaishi ya ukombozi wa mtu binafsi ambao hudhihirika kama nguzo za kukuzia uhuru wa binadamu unaofasili falsafa ya maisha. Masinde (2003) na kina Njogu na Chimerah (1999) wanasisitiza kwamba maumivu haya kifalsafa ndiyo dira ya ukombozi kutoka kwenye ngome ya maisha ya kutamausha anayoangazia Kezilahabi kwenye mashairi yake. Kezilahabi anaonyesha kwamba ukombozi wa kudumu ni nadra kupatikana katika maisha ya mwanadamu. Kwake maisha ni adhabu aliyopashwa binadamu, na ambayo hawezi kuikwepa kwa vyovyote vile. Harakati za ukombozi wa binadamu humtesa sana kiasi cha kutaka kujitoa kitanzi ili apate uhuru wa kudumu. Hii ndiyo tasnifu ya ukombozi anayoibua Kezilahabi kupitia kwa



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | Aug-2020|
Received: 05.08.2020; Accepted 09.08.2020; published on 31.08.2020 at www.editoncpublishing.org
Poyi, J.C., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

taswira ya kisu mkononi. Kwenye shairi la *Kisu Mkononi* (Kezilahabi, 1974a: 13), anayaona maisha kama yanayomtesa binadamu na kumkosesha amani. Hata hivyo, binadamu hana hiari kuyaishi yalivyo kwa sababu hatima yake tayari imeratibiwa. Maisha kwa mtazamo huu hufuata mkondo fulani ambao hauwezi kukiukwa. Yanaonekana kuendeshwa na nguvu fulani nje ya uwezo wa binadamu. Hii ndiyo hali ambayo Kezilahabi ameisawiri katika shairi la *Kisu Mkononi*:

> Wakati miaka inaibwa mmoja mmoja
> Kurudi nyuma, kusimama, kupunguza mwendo
> Siwezi, kama gurudumu nitajivingirisha
> Mtelemko mkali huu
> Lini na wapi mwisho sijui
> (Kezilahabi, 1974a: 13)

Katika ubeti wa kwanza, Msimulizi anasema kwamba kadri miaka inavyosonga ndivyo maisha yake yanavyozidi kuwa yenye vitisho vingi. Vitisho ambavyo vinamsukuma kuyamithilisha na mteremko mkali ambao hajui ama lini au wapi mwisho wake. Katika hali halisi, mteremko huu ni kadhia za maisha ambazo zinaweza kumwangamiza binadamu asipochukua tahadhari katika harakati za kujinusuru. Hata hivyo, mshairi hana hiari ila kufuata mkondo huo unaohatarisha maisha yake kwa kujivingirisha kama gurudumu. Hii ina maana kwamba mshairi yupo tayari kwenda popote ambapo maisha yatamwelekeza. Mshairi anaona harakati za ukombozi wake kuwa kama mteremko mkali wenye ghururi, vitisho na wenye kutamausha kwa anayedhamiria kushuka chini kwa sababu huenda ukamwangamiza. Ghururi na vitisho hivi kwa uhuru wake hajui ni lini na wapi utakuwa mwisho wake.

Katika ubeti wa pili, mshairi hana matumaini ya kujikwamua kutoka kwenye ukatili wa maisha. Anasema:

> Mbele chui mweusi, nyuma mwanga
> Nionako kwa huzuni vifurushi maelfu ya dhambi
> Kisu, maisha kafiri haya
> Kama kutazama nyuma au mbele
> Ni kufa moyo mzima!
> (Kezilahabi, 1974a: 13)

Chui mweusi anasawiri hatari inayomsubiri binadamu katika mchakato wake wa ukombozi. Mshairi amemtumia chui mweusi kuonyesha maisha yenye hatari. Kwa kuwa maisha yamesheheni hatari nyingi, ndivyo hivyo mchakato wa ukombozi ulivyojaa hatari nyingi ambazo zimesheheni maangamizi. Mshairi anaona afadhali maisha anayoyaishi yenye mwanga unaompa matumaini ya uhuru wenye mipaka. Mshairi anaelekea kuhunishwa kwa kuona kuwa maisha ni maelfu ya dhambi. Usemi ambao unadhihirisha maovu ya kila aina ya maisha ya halafu. Hali hii inamsukuma mshairi kusema kwamba, "*kutazama mbele au nyuma ni kufa moyo mzima.*" Usemi unaodhihirisha maisha ya baadaye kama yenye kukatisha tamaa. Usemi huu ni ishara tosha kwamba dunia ni uwanja wa fujo ambazo mshairi anaweza kuziepuka tu kwa kujitia kitanzi kwa kisu. Ingawa anaghairi nia yake na kukiri kwamba "*maisha kafiri*" kuonyesha kwamba hana budi ila kuyaishi yalivyo. Msimulizi hana matumaini ya kuboresha hali yake na kujikomboa dhidi ya ukafiri huu wa maisha.

Kwenye ubeti wa mwisho, mshairi anaghairi kujitia kitanzi ambacho kilionekana kumpa ahadi ya uhuru wa kudumu dhidi ya maisha yanayomtesa. Anasema:

> Sasa kama Simba-Mtu shauri nimekata
> Ya nyuma sana nisijali, ya mbele sana niyakabili
> Kwa ujasiri na uangalifu nitazunguka
> Nikifuata kamba kama ng'ombe aliyefungwa
> Kila mpigo wa moyo wangu



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | Aug-2020|
Received: 05.08.2020; Accepted 09.08.2020; published on 31.08.2020 at www.editoncpublishing.org
Poyi, J.C., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, Double –Blind Peer Reviewed Journal

Huu mpigo muziki wa maisha
(Kezilahabi, 1974a: 13)

Kwa kuwa uhuru anaoutafuta ni muhali kuupata, mshairi anaamua kuyakabili maisha kama Simba-mtu. Anajasiria kama Simba kuyakabili maisha yalivyo bila hofu yoyote. Namna maisha yalivyo kafiri, binadamu hana hiari ila kuyaishi vivyo hivyo. Msimulizi anaamua kuyaishi maisha haya kama ng'ombe aliyefungwa kamba ama mguuni ama shingoni. Kamba hapa inaibua dhana kwamba maisha yamemwekea mshairi mipaka kwa uhuru wake. Naye mshairi hana budi kuyaishi kwa mujibu wa sheria hizo za maisha zinazodhibiti uhuru wake. Ameshikamana na kusalia kucheza muziki wa maisha kama anavyokiri kwamba, "*kila mpigo wa moyo wangu ni mpigo muziki wa maisha*." (Masinde, 2003)

**Ukombozi unachosha na kuhofisha**

Ukombozi unachosha na kuhofisha Katika diwani ya *Kichomi*, Kezilahabi ameusawiri ukombozi kama mateso yanayoambatana na msako wa ukweli na uhuru ambao hauna mwisho. Msako huu wa uhuru kwa Kezilahabi hukadiriki kwa sababu uhuru wenyewe ni wa muda tu, na hivyo kuibua hisia za uoga na uchovu. Kwa kuwa mchakato huu wa kutafuta uhuru hufikia ukomo wakati wa mauko halisi, huishia kumchosha na kumwogofya anayeutafuta kama anavyoonyesha Kezilahabi kwenye shairi la *Nimechoka* (Kezilahabi 1974a: 34-35).

Kezilahabi anatumia uchovu kuusawiri mchakato mrefu wa kutafuta uhuru usio na mwisho. Njogu na Chimerah (1999) wakirejelea Sartre wanaandika kwamba, mtu huzaliwa au hujipata ametumbukia kwenye ombwe fulani bila yeye kujua. Ni juu yake kutafuta lengo la yeye kuishi ambalo litamkomboa kutoka kwenye udhalimu wa maisha. Hali hii ndiyo inayomkumba mshairi kwenye ubeti wa kwanza wa shairi la *Nimechoka*:

Nilivyofika hapa, na juu kupandishwa.
Na kwa hila gani, au, zilipofungwa
Ncha za waya hii ngumu ya maisha, sijui.
Lakini najiona nimening'inia kama ndege
Aliyenaswa na mtego wa mtoto mdogo.
Mimi, lakini, ni mwanadamu na akili zangu
Timamu. Ninaweza kudondoka, kama nikipenda
(Kezilahabi 1974a: 34)

Hajui alivyofika aliko wala aliyempandisha hapo. Amefungwa waya mgumu wa maisha usio na mwanzo wala mwisho. Haelewi sababu ya yeye kuishi katika hali hiyo ngumu ya maisha. Anakosa uwezo wa kujikwamua kutoka kwa maisha magumu, hali inayomfanya kujimithilisha na "*ndege aliyenaswa na mtego wa mtoto mdogo.*" Mchakato wa ukombozi unakuwa adhabu kali inayomuungulisha mshairi. Kama binadamu razini, anaamua kuishikilia licha ya maumivu anayoyahisi. Waya mgumu wa maisha unaonyesha hali ngumu ya kujikomboa anayopitia mshairi na ambayo hajui mwanzo wala mwisho wake. Mshairi ananing'inia kwenye waya huo mgumu wa maisha kama ndege aliyenaswa kwenye mtego wa mtoto mdogo kuakisi ukweli kwamba hana uwezo kujitoa kwenye mitego ya maisha ila kushikamana na hali ngumu ya maisha yake.

Mchakato wa mshairi kujikomboa unazidi kuwa wenye hatari nyingi zaidi katika ubeti wa pili anaposhindwa kujitoa kwenye waya mgumu wa maisha kwa kuhofia kudungwa na miti iliyochongwa kama mishikaki iliyokuwa chini yake:

Lakini naogopa chini yangu naona miti
Iliyochongwa ikifuata usawa wa waya hii,
Ikingoja kwa hamu, kama mishikaki kunichoma,
Kunitoboa na kufurahia kimya kimya
Uzuri wa kupita katika mwili mwororo wa binadamu,



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | Aug-2020|
Received: 05.08.2020; Accepted 09.08.2020; published on 31.08.2020 at www.editoncpublishing.org
Poyi, J.C., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, Double –Blind Peer Reviewed Journal

Lazima nishike kwa nguvu nisianguke kama kifurushi
Cha pamba cha mtoto mdogo kilichokwisha pimwa
(Kezilahabi 1974a: 34)

Wamitila (2002) anadai kwamba, wadhanaishi hutilia mkazo udhaifu wa binadamu ambaye hawezi kujikwamua katika hali fulani. Kwa jinsi hii, mshairi anashindwa kujinasua kutoka kwenye waya wa maisha na inambidi ashike kwa nguvu ili asije akaanguka. Kila hatua ya kiukombozi anayoichuka mshairi ni kichomi. Hali yake inaonyesha maisha yenye upweke, hofu na machungu tupu. Ukosefu wa usalama pale chini ambapo angejidondosha unamlazimisha mshairi kuyaishi maisha yanayomdhulumu yalivyo kwa sababu hana budi lau asije akaanguka kama *"kifurushi cha pamba cha mtoto mdogo kilichokwisha pimwa."*

Katika ubeti wa tatu, miti ya mshikaki iliyochongwa inauwekea uhuru wa kudondoka wa mshairi mipaka. Mishikaki hii inamsukuma mshairi kushikilia zaidi waya wa maisha ambao unaishia kumkata mikono na kuanza kuvuja damu:

Mikono inaniuma, na waya imekwishanikata vidole.
Damu imetiririka hadi kwapani; kujipanguza siwezi
Nimechoka. Kadiri niendeleavyo kuning'inia, ndivyo
Sura yangu ionyeshavyo vizuri alama za uchovu
Ninatazama huku na huko kuwatafuta wenye huruma
Lakini wanadamu wote wazima wanainamisha vichwa
Chini kama kwamba hawanijui; hata jamaa zangu!
(Kezilahabi 1974a: 34)

Damu ambayo inatiririka hadi kwapani inaelekea kusawiri dhiki ya maisha ya binadamu. Mshairi anakiri kuchoshwa na maisha. Uchovu ambao Schopenhauer (2000) anasema kwamba, ni ithibati kamili ya maisha yasiyo na thamani, kwa sababu uchovu unaashiria mateso na hisia za utupu wa maisha. Machungu ya waya mgumu wa maisha yanamfanya atokwe na machozi ambayo hana uwezo wa kupangusa katika ubeti wa nne. Shairi hili linaakisi itikadi kamili ya msimamo wa mshairi kuhusu maisha kama kichomi ambacho hawezi kustahimili tena. Uchovu huu unafanya mshairi alilie msaada wa wanajamii ambao hawamjali hata jamaa wake wakiwemo. Hali hii inaoana na madai ya wadhanaishi kuwa binadamu ni kiumbe pweke duniani asiye na yeyote wa kumshikilia. Mshairi anasema:

Ninaendelea kuning'inia kama picha iliyotundikwa
Katika shamba la mawele, na mwenye shamba
Huvuta waya kutoka nyumbani, itingishike kuwatisha ndege.
Machozi yananitoka, kuyapangusa siwezi.
Ninajitahidi kutoa sauti kwa nguvu:
"Jamani e! Nisaidie! Ng'oeni hivyo vitimbo!
(Kezilahabi 1974a: 34)

Kwa kuwa wadhanaishi hupinga uwezekano wa hatari na mizigo ya binadamu kupungua na kuwa mwepesi wa kubebeka, hushikilia kwamba hatari humzidia binadamu na kuyafanya maisha yake magumu na hatimaye kumwangamiza kwa kuwa maisha ni kifo cha polepole. Mwishoni mwa shairi hili, mshairi anaonekana kutoa tabasamu japo bado hatari ya vitimbo bado inamtesa. Anasema:

Ninaendelea kuning'inia. Nimechoka. Mikono


© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | Aug-2020|
Received: 05.08.2020; Accepted 09.08.2020; published on 31.08.2020 at www.editoncpublishing.org
Poyi, J.C., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, Double –Blind Peer Reviewed Journal

Inaniuma; hatari ya vitimbo. Vinacheka. Wanasali
Sasa wanaimba. Sitaki nyimbo zao; maana
Mimi bado nimening'inia na vitimbo having'oki.
Lakini polepole ninaanza kutabasamu.
Sijafikia hatua ya kucheka; maana nimechoka
Kichomi kimenipata na sijadondoka
(Kezilahabi 1974a: 35)

Mshairi anafunua tabasamu kuashiria kwamba ameanza kupata mwao kidogo wa namna ilivyo vigumu kupata uhuru. Tabasamu hii haidumu kwa sababu hajafikia kiwango cha kucheka ambacho kinaonyesha ufahamu kwamba uhuru unaopatikana si wa kudumu. Hii inatokana na ukweli kwamba furaha ya kudumu haiwezi kupatikana katika maisha ya binadamu. Na hata pale inapopatikana, huwa ni kwa muda mfupi tu. Mshairi anaonekana kupatwa na kichomi ambacho kinamtesa ijapokuwa hajadondoka yaani sio huru. Tabasamu anayoonyesha mshairi inaashiria ung'amuzi wa namna msako wa ukombozi ulivyo kipindi cha mateso. Waya mgumu wa maisha unaashiria dhiki na machungu yanayomkumba binadamu katika harakati za ukombozi. Mtu aliyening'inia anasawiri upweke na upekee wa binadamu asiye na yeyote wa kumwauni dhidi ya ukatili wa maisha. Vitimbo vinaonyesha hatari inayomsubiri binadamu katika mchakato wa kujikomboa. Watu wanaosali wanaibua mwelekeo wa wanajamii kuhusu nafasi ya dini katika maisha yao. Vichwa vyeupe ni ishara ya tanzia huku kichomi kikiashiria machungu na maumivu ya maisha ya binadamu dunia. Watu wanampuuza mshairi wanaashiria maadili ya kijamii yaliyozoroteka. Kwa msingi huu, Kezilahabi anakejeli dhima ya dini katika dunia yenye fujo. Hiki ndicho chanzo cha mshairi kuteseka na kufedheheka huku waumini wakijali maslahi yao. Chanzo ambacho kinamchosha na kuhofisha kwa hali zote.

**Ukombozi husakama na kuibua upweke**

Mchakato wa kutafuta uhuru unamsakama mshairi na kumfanya ahisi pweke. Dhana hii ni dhahiri kwenye shairi la *Fungueni Mlango.* Mshairi anasema:

Hewa kunikosa
Na jasho kunitoka ndani ya chumba
Kwa upweke
Ninajiona nimefungiwa.
Sioni madirisha lakini
Mlango wa karatasi uko mbele yangu
Ninaugonga kwa mikono
Kichwa na mabega
Mlango unatoa mlio kilio,
Lakini mwanadamu hatanifungulia.
(Kezilahabi 1974a: 23)

Katika ubeti huu, mshairi anasakamwa ndani ya chumba kwa kukosa hewa na jasho kumtiririka. Mshairi anajikuta yu pweke katika chumba ambacho amefungiwa na anachosema ni kwamba haoni madirisha isipokuwa mlango wa karatasi mbele yake. Juhudi za Mshairi kufungua kwa kugonga kwa mikono, mabega na kichwa hazifui dafu. Mshairi kukosa hewa ndani ya chumba kunaashiria maangamizi yanayotokana na ukatili wa maisha. Jasho linalomtoka linaelekea kuonyesha hali ngumu ya maisha inayomsibu Mshairi. Mlango wa karatasi ulioko mbele yake na ambao mwanadamu hawezi kumfungulia unaelekea kumaanisha kwamba Mshairi amenyimwa uhuru wa kuishi na wa utunzi. Chambilecho Gaudioso (2014) kwamba, Mshairi, kwa kushiriki katika utunzi wa mashairi na hivyo basi kuangamiza ulimwengu wenye kutamausha, hahisi huru duniani. Mshairi hahisi kana kwamba anajitegemea bali anaona hajielewi na kwamba ameachwa pweke katika hali inayomsukuma nje ya maisha na kuishi. Mshairi ametengwa na ni mpweke katika dunia ya kibinafsi. Hali ambayo inamtesa na kumtamausha.



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | Aug-2020|
Received: 05.08.2020; Accepted 09.08.2020; published on 31.08.2020 at www.editoncpublishing.org
Poyi, J.C., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, Double –Blind Peer Reviewed Journal

Mshairi anatokwa na damu puani, mdomoni na kichwani ambayo anaitumia kama wino. Anahisi uchovu mikononi, kichwani na mabegani lakini bado yupo kwenye mchakato wa kutafuta uhuru wake anaposema kwamba ataugonga mlango tena kama agongavyo mbuni kichwa mchangani. Anasema:

Damu
Damu puani, damu mdomoni,
Damu kichwani itumikayo kama wino.
Mikono, kichwa, mabega uchovu.
Kwa kichwa kama cha mbuni
Mchangani, tena ninaugonga
Lakini mwanadamu hatanifungulia.
(Kezilahabi 1974a: 23)

Hata hivyo bado Mshairi hatarajii msaada wa mwanadamu yeyote. Hali ambayo inaashiria kwamba yuko peke yake katika dunia ambayo haimjali. Kwa kuwa Mshairi yuko nje ya uwezekano wa wakati kwa sasa, wakati utunzi na kuishi katika dunia ni jinsi mbili tofauti za maisha, na hawezi kuishi katika dunia tena. Uhusiano wa Mshairi na dunia halisi umeharibika vibaya kiasi kwamba anatumia damu kama wino wa kuandika kama ishara ya mateso anayopitia. Mshairi amefungika katika utunzi kiasi kwamba hana wa kumwauni ijapokuwa ana matumaini utunzi wake utashuhudia alivyo.

Kwenye shairi hili, 'mlango' unaelekea kuwa ndio kizingiti kwenye ukombozi wa maisha na mawazo ya Mshairi. Damu na kelele katika ubeti wa mwisho wa shairi hili ina nafasi kubwa kidhanaishi kama ilivyo katika diwani nzima (Gaudioso, 2014). Katika diwani hii, ni wazi kupitia kwa Mshairi kwamba Kezilahabi ni mwathiriwa sana wa hofu ya maisha kutokana na kihoro cha ukombozi, jambo ambalo linadhihirika katika shairi lake la *Fungueni Mlango*. Kama binadamu asiyekuwa wa kawaida, aliamua kuwa kiumbe bunifu, ambaye alikuwa tayari kuishi peke yake na kutafuta uhuru wa utunzi wake. Gaudioso (2014) anasema kwamba mlango wa karatasi ulioko mbele ya Mshairi unamsaidia Kezilahabi kuibua ishara za damu, kelele na ng'ombe ambazo zina nafasi falsafa yake. Anasema:

Ninaona kizunguzungu
Ninapiga kelele kama
Ng'ombe machinjioni:
Fungueni mlango!
Mlango fungueni!
Lakini mwanadamu hatanifungulia.
(Kezilahabi 1974a: 23)

Ng'ombe machinjioni anaelekea kuibua dhana mbili muhimu za kidhanaishi: kwanza ni mandhari ya kifo cha Mshairi kama alivyo ng'ombe anayekufa machinjioni na pili inatumia lugha ishara na hususani kelele ya mnyama anayekufa kuonyesha mwisho wa maisha ambao inampa mshairi ahadi ya uhuru wa kudumu. Ng'ombe hapa anasimamia binadamu ambaye hana uwezo wa kujinasua kutoka kwenye pingu za maisha kutokana na udhaifu wake. Kezilahabi anaelekea kusema kwamba binadamu ni mnyama tu kwa sababu kama alivyo mnyama, binadamu ana sauti ambayo haiwezi kumwepusha kifo. Kelele ya kifo cha ng'ombe inamwonyesha ng'ombe mwenyewe kama anayekufa na kwamba lugha haiwezi kuusawiri ukweli kuhusu kifo na kuonyesha kikamilifu sababu za kelele hiyo. Sauti inaonyesha maisha yenye mateso, hisia, ukosefu wa ukamilifu uliomfanya Mshairi kuwa na huzuni na dhiki. Kwa kuwa kelele ni sauti bila maneno, inaelekea kuonyesha kifo cha maneno ambayo tena hayawezi kusema ukweli wa mauti. Maneno haya hayana maana kwa sababu hayawezi kuonyesha uduni wa maisha ya binadamu. Kupitia kifo chake, maneno yanaafikia upeo wa giza linaloashiria hali ya hatari ya maisha ya binadamu ambayo yanaonekana kumtesa.

Upweke huu unaomtesa Mshairi unaotokana na hisia za kutengwa katika harakati zake za kutafuta ukombozi, ambao pia ni uhuru, unamfanya ahisi namna ilivyo vigumu kwa kazi ya fasihi katika kumkomboa kutoka kwa hali



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

Volume: 02 Issue: 01 | Aug-2020|
Received: 05.08.2020; Accepted 09.08.2020; published on 31.08.2020 at www.editoncpublishing.org
Poyi, J.C., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, Double –Blind Peer Reviewed Journal

yake duni. Hali inayomsukuma Msimulizi kusema kwenye shairi la *Dhamiri Yangu* (1974a: 36) kwamba, "*Hapa nilipo sina uhuru*."

**Matokeo**

Makala hii inadhihirisha namna ukombozi na uhuru wa binadamu ulivyosawiriwa katika diwani hii. Imebainika wazi kwamba ukombozi wa binadamu umesheheni mateso yanayomchosha na kumwogofya binadamu na hatimaye kumsakama na kumwacha akiwa pweke. Maisha yamemwekea binadamu mipaka kwa uhuru wake na juhudi zake za kujikomboa kutoka katika silisili za mipaka hii huishia katika utamaushi. Harakati za binadamu za kutafuta ukombozi huwa kama safari ya kuzunguka kwenye duara na ambayo huelekea kuonyesha kwamba uhuru wake ni nadra kupatikana. Duara hili huyasawiri maisha ya binadamu ambayo kidhanaishi hayapigi hatua mbele wala nyuma bali yanaendelea kuzunguka mzunguko dhalimu wa dunia katili ambayo inamtesa binadamu. Mipaka hii ya maisha inaibua dhana kwamba, binadamu ni mfungwa na hana budi kuzunguka duara lile lile akifuata sera ya maisha kama yalivyo kwa sababu hawezi kujikomboa na kuwa na mkondo huru wa maisha. Yaani maisha yanafuata mkondo fulani ulioratibiwa na ambao hauwezi kukiukwa na yeyote. Binadamu hana hiari ila kuendelea kuishi yalivyo.

**Hitimisho**

Makala hii imeshughulikia usawiri wa ukombozi katika diwani ya *Kichomi*. Katika makala hii, sifa bainifu za ukombozi zilizofunuliwa ni idhibati tosha kuwa mchakato mzima wa ukombozi ni wenye kuchosha, kuogofya na ambao unamsakama na kumwacha binadamu akiwa pweke katika dunia isiyomjali. Uchanganuzi huu unauonyesha ukombozi kama mojawapo wa sifa bainishi ya falsafa ya Kezilahabi, ambayo huifanya kuwa falsafa ya uhuru yenye tafsiri nyingi zilizopambanuliwa kwenye makala hii. Hatimaye, usawiri huu wa ukombozi unadhihirisha wazi namna uhuru wa binadamu ulivyo muhali kupatikana na hata ikawa umepatikana, hauwezi kudumu. Haya yote yamefanikishwa kwa kuongozwa na nadharia ya udhanaishi. Makala hii ni mchango mkubwa kwa taaluma ya mijadala ya kiusomi kuhusu ushairi wa Kezilahabi, hususan falsafa yake ya maisha. Vilevile, yanafungua milango kwa uhakiki wa sifa nyingine bainishi zinazokuza nguzo kuu za falsafa hii ya maisha kwenye ushairi wa Euphrase Kezilahabi.

**MAREJELEO YA KIMSINGI**

Acquiviva, G. (2004). Jazanda ya Njozi Katika Baadhi ya Mashairi ya Euphrase Kezilahabi. *Swahili Forum* 11, 69-73.

Gaudioso, R. (2014). *Kuwako na Wakati: Mipaka ya Matumizi ya Lugha kama Hatua za Falsafa katika Mashairi ya Euphrase Kezilahabi*. Swahili Forum Xxi: 76-103

Gaudioso, R. (2015). Transferring and Rewriting Freedom in Euphrase Kezilahabi. *Nordic Journal of African Studies* 23(2), 63–89

Hassan, M.A. (2013). *Kuchunguza Vipengele vya Fani katika Mashairi ya Kiswahili: Ulinganishi wa Mashairi ya Euphrase Kezilahabi na Haji Gora Haji.* Tasnifu ya MA, chuo kikuu Huria Tanzania. Haijachapishwa.



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

**Volume: 02 Issue: 01 | Aug-2020|**
**Received: 05.08.2020; Accepted 09.08.2020; published on 31.08.2020 at www.editoncpublishing.org**
**Poyi, J.C., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili., Double –Blind Peer Reviewed Journal***

Karama,M. na Mwamzandi, I. (2019). Ushairi wa Kezilahabi ni Ushairi wa Nabhany: Ushahidi kutoka Uchanganuzi wa Umbo la Shairi la Wanajadi. *East African Journal of Swahili Studies*, 4(1),

Kezilahabi E. (1974). *Kichomi*. London: Heinemann Educational Books (EA) Ltd

Masinde, E. (2003). *Ushairi wa Kiswahili: Maendeleo na Mabadiliko ya Maudhui*. Tasnifu ya uzamifu: Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Mbatiah, M. (1997). *Mienendo mipya katika uandishi wa Kezilahabi*. Makala haya hayajachapishwa.

Mlacha, S.A.K. (1987). *The Portrayal of Cultural Conflict in Kiswahili Prose Fiction: A Structural Study of the Novels of Euphrase Kezilahabi*. Unpublished Phd Thesis, SOAS, University Of London.

Mulokozi, M.M. (2017). Utangulizi katika Flavia Aiello na Roberto Gaudioso, *Ushairi na Uhuru: Mkusanyiko wa tungo za Abdilatif Abdalla na Euphrase Kezilahabi*. Napolli

Mulokozi, M.M., (1992). *Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Njogu, K. na Chimerah, R. (1999) *Ufundishaji wa Fasihi, Nadharia Na Mbinu* .Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Omary M. (2011). *Siasa Katika Ushairi wa Kezilahabi: Uchanganuzi wa Karibu Ndani Na Dhifa.* Tasnifu Ya MA Kiswahili, Chuo Kikuu Cha Dar Es Salaam.

Ranne, K. (2006). *Drops that Open Worlds, Images of Water in the Poetry of Euphrase Kezilahabi.* MA Thesis, University Of Helsinki.

Sartre, J-P (1970). *Existentialism and humanism*. London: Eyre Methuen.

Senkoro, F.M. (2006). Fasihi ya Kiswahili ya Majaribio: Makutano ya Fasihi Simulizi na Fasihi Andishi. *African Journals Online*, 4,(1), (2006)

Schopenhauer, A. (2000). On the Vanity of existence. In E, D. Klemke (Ed). *The meaning of life* (2nd ed). New York: Oxford University Press.

Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na vipengele vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Wamitila, K. W. (2008). *Dibaji*. In Kezilahabi Euphrase, 2008: *Dhifa*. Nairobi: Vide Muwa.

Wamitila, K. W. (2006). *Kamusi ya Ushairi*. Nairobi: Vide Muwa Publishers Limited.

Wamitila, K. W. (2008). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide-Muwa Publishers Ltd.



**© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org**